

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

☎ Simu: Na : 026 -2702647
☎ Faksi Na : 026 – 2702203
☎ Email:mkurugenzi@iringamc.
go.tz
☎ Tovuti:www.iringamc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa,
S.L.P 162
IRINGA.

23/4/2018

TAARIFA KWA WANANCHI

**MANISPAA YA IRINGA KUTOA MKOPO WA SHILINGI MILIONI 140 KWA
VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA.**

Manispaa ya Iringa inatarajia kutoa kiasi cha shilingi 140,000,000/= kwa vikundi 42 vya wanawake na vijana tarehe 24/4/2018 siku ya Jumanne katika ukumbi wa Community Centre, ikiwa ni kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2017/2018.

Katika mkopo huo kiasi cha shilingi 100,500,000/= kitatolewa kwa vikundi 30 vya wanawake ambayo ni sawa na asilimia 48 ya fedha iliyotengwa kwa vikundi vya wanawake na shilingi 39,500,00/= itatolewa kwa vikundi 12 vya vijana ambayo ni sawa na asilimia 19 ya fedha iliyotengwa kwa vikundi vya vijana.

Jumla ya wanachama 584 watanufaika na mkopo huo ambapo katika hao wanawake ni 480 na vijana ni 104 kutoka kata zote 18 zilizo katika Manispaa ya Iringa.

Aidha katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Manispaa ya Iringa imetenga kiasi cha shilingi 418,082,700/= ambayo ni asilimia 10 ya mapato ya ndani kwaajili ya mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake

Mkopo huo unatarajiwa kutolewa katika ukumbi wa Community Centre kuanzia saa 4:00 asubuhi kesho siku ya jumanne.

Imetolewa na

Sima Bingileki

Afisa Habari Manispaa ya Iringa.